JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA BUKOBA.

SHULE YA SEKONDARI KAHORORO,
S. L. P 198,
BUKOBA.

MARCH……/…../2022

MKOA WA KAGERA
SIMU N0: 0755 – 300656, 0786528610

E-mail: ***kahororosec@gmail.com***

KUMB. Na. KSS/I/C/27/35

MWANAFUNZI ……
……..
S.L.P ……
……

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KAHORORO KIDATO CHA CHA 5 …….. MWAKA 2022/2023**

UTANGULIZI:

- **UNAOMBWA USOME FOMU HII, HASA SHERIA ZA SHULE KWA UMAKINI SANA, IKIWEZEKANAUMSHIRIKISHE MZAZI/MLEZI WAKO KWA SABABU BILA NIDHAMU HAKUNA TAALUMA BORA.**

1: **TAARIFA**:
Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa / umeruhusiwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka **2022**. Shule hii ni ya Bweni na ni ya wavulana tu.

(i) Shule ya Sekondari Kahororo ipo umbali wa **Km 3** Kaskazini Mashariki kutoka stendi kuu ya mabasi mjini **Bukoba**, usafiri wa kuja shuleni ni kwa njia ya taxi.
(ii) Shule itafunguliwa Tarehe **05/07/2021** na unatakiwa kuripoti tarehe hiyo. Mwisho wa kuripoti ni ……..

2: **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**:
SARE YA SHULE:
(a) Unatakiwa kufika na mahitaji yafuatayo kwa ajili ya Sare ya Shule.
(i) Shati mbili za rangi nyeupe mikono mifupi, kitambaa cha "**Tetron**"
(ii) Suruali mbili rangi nyeusi kitambaa kifaacho kushona suti, kisiwe na mistari yoyote (suruali isibane mwili) – ufike umezivaa siku ya kuripoti. Kama inawezekana ashone zaidi ya mbili.
(iii) Viatu vya ngozi vya rangi nyeusi vyenye uzi (gidan) ambavyo havikuchongoka, soksi nyeupe au nyeusi jozi nne (pea mbili za viatu)
(iv) Mkanda mweusi usiozidi upana wa senti mita nne (sm 4) na kifungo cha mbele (buckle) kisiwe na urembo wowote.
(v) Aje na sweta ya rangi ya bluu yenye shingo la ''**V**''
(vi) Tai yenye rangi ya damu ya mzee yenye michirizi ya njano
Angalizo: Ukikosa huko (**Sweta,T-shirt na tai**) zinapatikana huku Bukoba madukani ,ukifika shuleni utaelekezwa maduka yanayouza hayo mahitaji.

(vii) T-Shirt mbili (2) rangi ya kijivu shingo ya mviringo au duara ISIYO NA MAANDISHI YOYOTE.

(b) **MAVAZI YA MICHEZO NA NGUO ZA KAZI ZA MIKONO**:

(i) Bukta moja rangi nyeusi au bluu.
(ii) Unaruhusiwa kuvaa T –shirt ya Shule wakati wa kazi za nje.
(iii) Wanaocheza mpira wa mikono waje na jezi yenye rangi ya bluu.
(iv) Viatu vya raba rangi nyeusi.

(c) **MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANATAKIWA KULETA SHULENI**:

- Ufika Shuleni unatakiwa kuwa na vifaa vya kazi za usafi na Elimu ya kujitegemea kama ifuatavyo:-
  (i) Mfagio mmoja wa ndani na mpini wake
  (ii) Ream (**2**) mbili za **A4** (karatasi nyeupe za photocopy)
  (iii) Mfagio wa nje mgumu **(chelewa).**

(d) **MAHITAJI BINAFSI**:

- Unatakiwa ulete vifaa vifuatavyo vitakavyokusaidia katika maisha ya kila siku hapa shuleni.
  (i) Bakuli, sahani, kikombe, kijiko.
  (ii) Godoro moja la sponji ukubwa wa futi sita (6) kwa futi mbili na nusu. (godoro imara lililofunikwa)
  (iii) Pasi ya mkaa kwa ajili ya kunyoshea nguo.
  (iv) Shuka mbili rangi ya pinki.
  (v) Blanket moja nzito.
  (vi) Vitabu vya masomo ya tahasusi unayososoma (orodha imeambatanishwa)
  (vii) Dissecting kit kwa wanafunzi wanaosoma Baolojia
  (viii) Bima ya afya ni lazima (aioneshe siku ya kuripoti) au afike shuleni na Tshs 50,400 Ili akatiwe **BIMA** katika ofisi za **BIMA** za **Mkoa**
  (ix) Chandarua yenye pembe nne rangi nyeupe (Mazingira ya shule yana mbu wengi).
  (x) Mto na foronya mbili (rangi ya pinki).
  (xi) Kamusi ya Kiingereza (English – English Dictionary).
  (xii) Mkebe wa vifaa vya Hisabati na ('Scientific calculator' – silent nonprogrammable with functions ranging from fx – 82 Ms to fx – 991Ms.(Kwa wale wanaosoma Sayansi na Hesabu).
  (xiii) Madaftari (Counterbooks) yasiyopungua 10, madaftari ya kawaida na graph kwa ajili ya mazoezi.
  (xiv) Jalada (file cover) la kutunzia majibu yako ya mitihani (examination scripts).
  (xv) Vifaa vya usafi (mswaki, dawa ya viatu, brashi, kioo, kitana, kandambili n.k.)
  (xvii)Taulo na nguo za kulalia. (iwe kaptula nyepesi nyeusi na fulana nyeupe)
  (xviii) Karatasi za kutumia maliwatoni (toilet paper) tano.
  (xix) Sanduku imara na kufuli madhubuti kwa ajili ya kutunzia mali zako.
  (xx) Dumu la lita 5 la kutunzia maji ya kunywa, na beseni au ndoo ya kufulia.
  (xxi) Rain boots rangi nyeusi (kwa matumizi ya wakati wa mvua na usafi) na mwavuli

N.B. **USILETE NGUO NYINGINE ZOZOTE TOFAUTI NA SARE YA SHULE**, (ukipata utata fika shuleni na mzazi/mlezi siku ya kuripoti ili upate ufafanuzi zaidi) au wasiliana na mkuu wa shule kwa maelekezo zaidi. (anaweza kuja na suruali nyeusi nne ili zimsaidie kubadilisha)

3. (A). **ADA NA MICHANGO MBALIMBALI**:

Ada ya Shule kwa mwaka ni Shilingi 70,000/= (Elfu sabini). Unatakiwa kulipa kiasi cha

(i) Shilingi 35,000/= kwa kila muhula au (70,000/= kwa mwaka) na kukabidhiwa stakabadhi kabla ya kusajiliwa shuleni. Pia utatakiwa kulipia Mambo yafuatayo:-
(ii) Shs. 5,000/= kwa ajili ya tahadhari ya uharibifu wowote utakaojitokeza Shuleni **(hairudishwi)**
(iii) Shs. 30,000/= kwa ajili ya mfuko wa ulinzi, wapishi na vibarua wengine.
(iv) Shs. 2,000/= kwa ajili ya Nembo ya Shule.
(v)Shs. 15,000/= kwa ajili ya kuchangia ununuzi wa madawa kwa ajili ya huduma ya kwanza

(kwa mwaka).

(vi) Shs.6, 000/= kwa ajili ya kitambulisho cha shule na usajili.
(vii) Shs.20, 000/= kwa ajili ya kuchangia samani na ukarabati mdogo.
(viii)Shs.20, 000/= kwa ajili ya kuchangia maendeleo ya taaluma na uendeshaji (kwa mwaka)
(ix) Shs 20000/= kwa ajili ya mtihani wa kujipima ngazi ya mkoa /kanda

3. (B). Fedha zote hizo zilipwe katika Akaunti ya Shule yenye taarifa zifuatazo.

KAHORORO SECONDARI SCHOOL FUND,
N.M.B. TAWI LOLOTE LILILOKARIBU NA NYUMBANI KWAKO,
ACCOUNT NUMBER 31801200094

- Michango YOTE ilipwe kwenye Akaunti **Na. 31801200094 KAHORORO SECONDARY SCHOOL**

(i) Hakikisha unalipia benki ya **NMB** iliyo karibu na nyumbani fedha yote ya ada (kwa muhula au mwaka mzima) pamoja na michango yote iliyoorodheshwa hapo juu, **hatutapokea pesa taslimu**. Fedha yote ilipwe benki ya **NMB** wiki moja kabla mwanafunzi hajaripoti shuleni kwa ajili ya maandalizi. Ukija na pesa taslimu hutapokelewa.Akaunti zote ziko **NMB**.

(ii) Nakala ya stakabadhi ya kulipia Benki (bank pay in slip) iwasilishwe Shuleni kwa ushahidi siku ya kuripoti ili upewe risiti.

NB: Kumbuka kuandika majina ya mwanafunzi katika pay slip ya benki ili iwe rahisi kutambua mlipiwaji na kumpa risiti wakati amelipoti shule.

4. **HATI NA NYARAKA MBALIMBALI:**

(i) Unatakiwa kuleta picha (**6**) za rangi ukubwa wa Passport ukiwa umevaa shati jeupe, picha zenye ndevu, nywele ndefu au mkufu hazitakubalika.
(ii) Unatakiwa ufike na nakala ya cheti cha kuzaliwa (**Birth Certificate**) au Hati ya kiapo (**Affidavit**) ili kudhibitisha uraia wako.
(iii) Utatakiwa kupimwa afya yako katika Hospitali ya Serikali. Fomu hiyo imeambatanishwa na maagizo haya. Ijazwe kwa ukamilifu na kukabidhiwa Shuleni siku ya kuripoti.
(iv) Umetumiwa Fomu ya Maelezo Binafsi ambayo utaijaza na kukabidhi Shuleni siku ya kuripoti. Huu ni mkataba kati ya shule, mwanafunzi na mzazi.
(v) Maagizo haya yameambatanishwa na Fomu ya makubaliano kati ya Shule na Mzazi/Mlezi. Ijazwe kikamilifu na kuletwa shuleni utakaporipoti kuanza masomo.
(vi) Uje na hati ya matokeo ya Kidato cha Nne **2021** (**Result Slip**)

5.0 **SHERIA ZA SHULE KWA WANAFUNZI**.

Kila Mwanafunzi anayo haki ya kupata masomo yanayotolewa katika Shule hii. Mwanafunzi anaweza kujinyima haki hiyo kwa kushindwa kufuata sheria na kanuni za shule kwa ujumla.Sheria na kanuni zifuatazo zina malengo ya kumlea mwanafunzi kimaadili na kumuwezesha kila mmoja kuishi kwa amani ili afikie kikamilifu lengo lake la kuwa shuleni.

5.1 MIPAKA YA SHULE:

Mipaka ya Shule ni mwisho wa viwanja vya michezo na mashamba ya shule, Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya maeneo ya hayo bila ruhusa ya mwalimu. Hairuhusiwi kutembelea vijiji vinavyozunguka shule bila kibali.

5.2 RATIBA YA SHULE.

Ratiba ya shule inajumuisha shughuli za masomo ndani na nje ya darasa, michezo, uzalishaji mali pamoja na utaratibu mzima unaoonyesha mwanafunzi anatakiwa kufanya nini, kuwa wapi na kwa wakati gani. Mwanafunzi atachukuliwa kuwa ana hatia akienda kinyume na ratiba ya shule bila idhini.

5.3 <u>SARE YA SHULE</u>:

Sare ya shule ni kama ifuatavyo:-

(a) Suruali safi nyeusi (Siyo mtumba, isiyobana mwili).

(b) Shati safi jeupe (tetron) la mikono mifupi na **mikono mirefu kwa viranja tu**, linalochomekwa vizuri ndani ya suruali. Lazima liwe na Nembo ya shule pia lisibane mwili.

(c) Viatu vyeusi vya ngozi vilivyotunzwa kwa unadhifu. (pea zaidi ya mbili)

(d) Soksi safi nyeupe, au nyeusi. (Pea zaidi ya mbili)

Sare ya shule itavaliwa wakati wote wa masomo, Baraza, mihadhara, na wakati mwanafunzi anapokwenda nje ya mipaka ya shule kama vile **Kanisani, Msikitini** n.k. T-shirt ya shule ivaliwe ndani ya shule wakati usio wa masomo, na sweta ivaliwe wakati wa baridi tu. Majaketi, Makoti, kofia na mapambo mengine haviruhusiwi kuvaliwa kabisa pamoja na sare ya shule. Huruhusiwi kuleta nguo nyingine tofauti na sare ya shule. Siku ya kusajiliwa uje umevaa sare ya shule (sharti jeupe na suruali jeusi).

❖ **HIVYO ATAKAYEONEKANA NA MAVAZI MENGINE TOFAUTI NA YALIYOAINSHWA HAPO JUU ATANYANG'ANYWA NA KUCHUKULIWA HATUA ZA KINIDHAMU. UTAVAA SARE YA SHULE WAKATI WA KWENDA NA KUTOKA LIKIZO (SHATI JEUPE AU T-SHIRT).**

5.4 <u>HESHIMA</u>.

(a) Kila mwanafunzi hana budi kuonyesha tabia njema kwa kila mtu. Lazima Mwanafunzi ajiheshimu kama anavyotarajia kuheshimiwa yeye.

(b) Mwanafunzi lazima asimame na kusalimu kila mwalimu, mfanyakazi asiye mwalimu au mtu anayemzidi umri anapopita,. Anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mkutano na kuwa heshimu wanafunzi wenzake**.**

- **<u>Epuka nidhamu ya woga, jitahidi uwe na nidhamu halisi (Self discipline)</u>**

(c) Lugha ya upole, utii na ustaarabu ndiyo inayoruhusiwa katika mawasiliano shuleni. matusi na kauli zisizozaheshima zitamsababishia mwanafunzi kupewa adhabu au kurudishwa nyumbani.

(d) Ugomvi, kupigana au fujo za aina yoyote ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote.

(e) Kila mwanafunzi anatakiwa kuitikia mara moja wito wa kengele, filimbi, ujumbe au ishara ya kuitwa kwa kukimbia mahali aliko mkuu aliyemita.

(f) Inabidi mwanafunzi kunyoosha mkono na kusimama anapouliza/anapojibu swali au hoja yoyote.

(g) Ni muhimu kuwa kwenye mstari wakati wa kupokea huduma au wakati wa mikusanyiko.

(h) Kila mwanafunzi anawajibika kuheshimu bendera ya Taifa na alama rasmi zinazotambuliwa na nchi yetu (Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa, Fedha ya Tanzania, Picha ya Rais, n.k.)

(i) Mwanafunzi kama raia yeyote, anapaswa kuheshimu tofauti za imani, siasa, mila na desturi za raia wengine kama msingi wa kujenga jamii yenye amani, umoja na mshikamano wa kitaifa. **ATAKAYEBAGUA WENZAKE KWA MISINGI YA DINI AU KABILA, NA KUVURUGA AMANI YA KITUO ATAFUKUZWA SHULE MARA MOJA; "SHULE NI YA SERIKALI NA HAIENDESHWI KWA MISINGI YA DINI. WANAFUNZI WANARUHUSIWA KUABUDU/KUFANYA IBADA BILA KUATHIRI UTARATIBU WA SHULE.MASWALA YOTE YA KIDINI YAPITIE KWA WALIMU WALEZI AU MAKAMU MKUU WA SHULE.**

(j) Ni lazima kuheshimu kiongozi mwanafunzi aliyepewa madaraka hayo kihalali. Viranja wote wanastahili kuheshimiwa kwa sababu wanafanyakazi kwa niaba ya Mkuu wa Shule. Atakayewadharau atapewa adhabu.

5. 5. <u>MAHUDHURIO</u>:-

(a) Kila mwanafunzi analazimika kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa**.**

(b) Hairuhusiwi kulala bwenini au kukosa vipindi vyote bila ruhusa ya maandishi kutoka kwa mwalimu wa zamu.

(c) Kushiriki katika kazi za uzalishaji mali, usafi, michezo, mazoezi ya viungo, midahalo mikutano ya shule ni jambo la lazima kwa kila mwanafunzi.

(d**) Atakayeshindwa mitihani kwa uzembe binafsi atapewa adhabu (Alama za ufaulu ni wastani wa alama 50) au "Division I, II na III." Ukipata "Division IV" au "Division O" utapewa adhabu.Ikibidi mzazi atashirikishwa kwa kufika shuleni.**

5.6. KANUNI ZA BWENI:

(a) Ni kosa kubwa kwenda nje ya shule bila ruhusa ya mwalimu.
(b) Kuondoka shuleni na kulala nje ya bweni ni kosa kubwa sana
(c) Lazima mwanafunzi aliyepewa ruhusa kwenda nje ya shule arudi katika muda uliopangwa na kuripoti kwa mwalimu wa zamu (**kabla ya saa 12:00 jioni).**
(d) Mwanafunzi mgonjwa anapaswa kutoa taarifa kwa mwalimu wa zamu kabla ya kuchukua hatua yoyote ile. Taarifa itolewe mapema kabla hali haijwa mbaya.
(e) Hairuhusiwi kujipikia chakula isipokuwa kwa kibali maalum cha mwalimu wa chakula .
(f) Lazima mwanafunzi awe ndani ya chumba chake (alichopangiwa) saa ya kulala.
(g) Chakula kitatolewa tu kwa wakati uliopangwa isipokuwa kwa sababu maalum.
(h) Hairuhusiwi kumkaribisha bwenini mgeni yeyote kutoka nje ya shule.
(i) Ni marufuku kutunza silaha ya aina yoyote (**Mfano: kisu, rungu, n.k**.) bwenini.
(j) Kelele haziruhusiwi na kuzomea wapita njia ni marufuku.
(k) Hakuna ruhusa ya kutunza chakula bwenini.
(l) Kila mwanafunzi ashiriki kufanya usafi wa eneo na bweni lake. Wenye chumba kichafu wataadhibiwa.
(m) Mwisho wa kuwa nje ya shule ni saa **12:00 jioni (Roll call – time**).

5. **USAFI**:

Kila Mwanafunzi lazima ajitahidi kutunza usafi wa mwili na mavazi yake, maeneo ya shule na majengo. Utupaji taka taka na matumizi ya choo, bwalo na mabweni vizingatie kanuni za afya. Kufuga kucha, ndevu au nywele ndefu ni marufuku. Kila mwanafunzi atashiriki kufanya usafi wa mazingira ya shule na kuhakikisha shule ni safi mda wote.

6. **SEHEMU MAALUM**:

Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum.

(a) Ofisi za shule na chumba cha walimu (Staff Room).
(b) Maabara za shule
(c) Jiko la shule
(d) Nyumba za wafanyakazi / walimu
(e) Maeneo ya starehe (Vilabu vya pombe, disko) na nyumba za kufikia wageni.
(f) Vijiji vinavyoizunguka shule, labda kwa ruhusa ya Makamu Mkuu wa Shule.

7. **MIKUTANO:**

Mikutano ya wanafunzi itaendeshwa kwa utaratibu mzuri chini ya ushauri wa mwalimu wa darasa, bweni au mwandamizi anayehusika na hoja inayojadiliwa. Muhtasari wa mkutano ukabidhiwe Ofisi Kuu ili kuhifadhiwa katika jalada linahusika. Mikutano yote ipate kibali kutoka kwa walimu walezi.

8. **MAWASILIANO**:

(a) Barua za kiofisi zinazotumwa nje ya shule lazima zipitie kwa Mkuu wa Shule.
(b) Wanafunzi wagonjwa washauriane na Makamu Mkuu wa Shule inapolazimika kwenda nyumbani.
(c) Kwa sababu za kimalezi, mwanafunzi haruhusiwi kumiliki "**simu ya mkononi**" anapokuwa shuleni, ukibainika kumiliki simu utarudishwa nyumbani na hatua nyingine za kinidhamu zitafuata.(Huruhusiwi kuweka taarifa zako,picha kwenye mitandao ya kijamii,ukigundulika utapewa **adhabu**).

9. **AFYA NA MATIBABU**.

Kila mwanafunzi atachangia **Tsh.15,000/=** kila mwaka kwa ajili ya kununulia madawa ya huduma ya kwanza ,ikitokea mwanafunzi akalazwa na kutibiwa kwa gharama kubwa mzazi atalazimika kuzilipa.

Hiki kiasi cha Tshs.15, 000/= ni za kununua madawa tu. Hazitatumika kwa matibabu anapolazwa hospitalini inashauriwa mzazi amkatie **Bima ya Afya mtoto wake** ili apate matibabu kirahisi.

10. **MALI YA UMMA**:
Lazima kutumia majengo, samani, umeme, maji na mali nyingine kwa uangalifu ili kupunguza gharama. Ili kuongeza usalama na kuwezesha mali kudumu, mwanafunzi atalazimika kulipia uharibifu wa kimakusudi wowote kama vile kuchubua nyaya za umeme na kuharibu miundombinu ya mfumo wa umeme.**Hivyo atakayekutwa anamiliki simu atagharimia uharibifu kabla ya kufukuzwa**. Ukiharibu mali yoyote ya Shule makusudi utalazimika kuilipa na kupewa adhabu.

11. **ADHABU**:
(a) Mwanafunzi akithibitika kufanya makosa kwa mujibu wa taratibu za shule atapewa adhabu kulingana na ukubwa wa kosa na pia kulingana na mamlaka aliyonayo mtoa adhabu (Kiranja, Mwalimu, n.k.).
(b) Mwanafunzi haruhusiwi kukataa adhabu iliyotolewa baada ya kosa kuthibitika.
(c) iwapo mwanafunzi hakuridhika na adhabu iliyotolewa atapeleka malalamiko yake ngazi ya juu baada ya kufanya adhabu. **N.B.USIGOME KUFANYA ADHABU**.
(d) Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha adhabu ya kufukuzwa shule.

(i) Wizi (ii) Utumiaji wa Pombe, Sigara, Bangi, Tumbaku na Mirungi
(iii) Ugomvi (iv) Utoro (v) Uasherati (vi) Kuandaa / kushawishi au kushiriki katika Mgomo (vii) Kukataa adhabu (viii) Makosa ya jinai (ix) Kuoa au kusababisha mimba
(x) Kuharibu mali ya umma kwa makusudi (xi) Kudharau bendera ya Taifa
(xi) Kusababisha madhara ya mwili kwa makusudi (xiii) Kumiliki simu ya mkononi ukiwa shuleni.

NB: ATAKAYE KUTWA NA SIMU ATAFUKUZWA SHULE NA ATALAZIMIKA KULIPA SH. 50, 000/= KUGHARAMIA UHARIBIFU WA NYAYA ZA UMEME WAKATI WA KUCHAJI SIMU.

(xiv) Kutohudhuria darasani na kutofanya mitihani
(xv) Kuvunja amani kwa misingi ya udini,ukabila na itikadi za vyama vya kisiasa
(xvi) Kushindwa kubadilika baada ya kuwa na makosa zaidi ya mara tatu.
(xvii) Kumdharau mfanyakazi/Mwalimu wa shule hii.
(xviii) **Kutozingatia masomo na kutofanya mitihani**.

12. **MWISHO**:
Binadamu hutofautiana na mnyama kwa sababu anaongozwa na sheria na taratibu zinazotawala utashi wake. Vile vile binadamu hupenda kuheshimiwa. Ni lazima kuheshimu sheria, kuheshimu watu wengine ili kuweza kutunza heshima yako mwenyewe.

"TUKUBALI KUFUATA SHERIA BILA SHURUTI ILI TUFIKIE MALENGO YETU YA ELIMU"

13. **MENGINEYO**:-
(a) Mwanafunzi hataruhusiwa kubadili jina tofauti na lile lililoandikwa kwenye maagizo haya.
(b) Mwanafunzi atapokelewa Shuleni katika saa za kazi kuanzia saa **2:00** asubuhi hadi saa **12:00** jioni(atakayechelewa awasiliane na uongozi wa shule kwa njia ya simu)
(c) Simu kwa ajili ya mawasiliano inapatikana Shuleni katika Ofisi ya Makamu Mkuu wa Shule.

Kwa niaba ya Shule ya Sekondari Kahororo, ninakupongeza kwa kupewa nafasi hii ya masomo, na ninatumaini kuwa utaitumia kujiendeleza wewe mwenyewe na Taifa kwa ujumla.

'WANAFUNZI WANAOSOMA KWA BIDII NA KUFUATA SHERIA ZOTE ZA SHULE HUFANIKIWA NA KUFAULU MITIHANI YA MWISHO'.

14. **USHAURI WA ZIADA**:

1. Uje Shuleni kwa lengo moja tu la kusoma.

2. Ukizingatia na kufuata sheria za Shule utaishi vizuri na walimu wako watapata muda mwingi na hamu ya kukusaidia.

3. Epuka vikundi vyenye nia mbaya na ukivibaini toa taarifa kwa Mkuu wa Shule.

4. Usifuate mkumbo, ukifuata baadaye utajuta.

5. Kumbuka elimu yako itasaidia ukombozi wako binafsi, familia yako na taifa kwa ujumla, hivyo tumia muda wako mwingi kujisomea kuliko kufanya vitendo visivyo na tija.
6. Maisha ya shule ni "**safari ndefu**".Hivyo unashauriwa kuvumilia na kujituma.

7. Shuleni siyo sehemu ya kustarehe, ni sehemu ya **kusoma na kufanya kazi.**

8. **Ukiwa na tatizo lolote omba ushauri kwa mkuu wa shule au walimu wengine kabla ya kuchukua maamuzi yoyote hata hivyo tuna kitengo cha ushauri hapa shuleni**

'KARIBU SANA KATIKA SHULE YETU'.

.....
MALICK O.OGAMBAGE
MKUU WA SHULE

ANWANI: ……..
……
……
TAREHE: ……

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI KAHORORO,
S.L.P 198,
BUKOBA.

FOMU YA KIAPO:

Mimi ni mwanafunzi ninayeishi …… toka Shule ya Sekondari …….. iliyoko Wilaya ya …….. ……. Mkoa wa …….. kwamba nimesoma na kuelewa maagizo na sheria za Shule hii na ninaahidi kuzingatia kukamilifu pamoja na kanuni zingine zitakazotolewa mara kwa mara shuleni. Endapo nitabainika kuwa nimekiuka sheria za shule, niko tayari kwa adhabu yoyote nitakayopewa, hata kufukuzwa shule.

Kama unakubali uthibitishe kwa maandishi.

i. Jina la Mwanafunzi: …….
Sahihi: …….
Tarehe: ……

ii. Jina la Mzazi / Mlezi : …….
Namba ya simu: …….
Sahihi: ……
Tarehe: ……..

iii. Jina la Mwenyekiti / Afisa Mtendaji wa Mtaa / Kitongoji ……
Anwani: ……
Sahihi: ……..
Muhuri wa Ofisi: …….
Tarehe: ……

KUMBUKA:

- BODI YA SHULE HII NA UONGOZI WA SHULE KWA UJUMLA UNAKUTAKA UZINGATIE SHERIA ZA SHULE NA UFANYE KAZI ILIYOKULETA YA KUSOMA. HATUTASITA KUKUONDOA SHULENI AU KUKUTAKA ULETE MZAZI WAKO PINDI UTAKAPOSHINDWA KUTII SHERIA ZA SHULE. MZAZI UNAOMBWA KUTOA USHIRIKIANO KATIKA MALEZI.

MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili **(kama lilivyo kwenye Result slip yako ya Form IV)**:

2. .....
3. Anwani ya nyumbani: .....
4. Tarehe ya kuzaliwa: ..... mahali ulipozaliwa; Kijiji: ..... Kata: ..... Wilaya: .....
5. Shule ya Sekondari ulipotoka: ..... Anwani: .....
6. Dini: ..... Kabila: .....
7. Taja Shirika,Mzazi,Mlezi au Mfadhili atakayekulipia Karo
   (i) Jina .....
   (ii) Simu :.....
8. Uraia: Mtanzania/Si Mtanzania
9. **Jamaa katika familia**:
   a) Jina la Baba: .....
      Anwani: .....
      Anaishi/Haishi: .....
      Kazi yake: .....
      Namba ya Simu: .....

   b) Jina la Mama: .....
      Anwani: .....
      Anaishi/Haishi: .....
      Kazi yake: .....
      Namba ya Simu: .....

   c) Jina la Mlezi: .....
      Anwani ya Mlezi: .....
      Uhusiano wake na wewe: .....
      Kazi yake: .....
      Namba ya Simu: .....

   d) Idadi ya Kaka: .....
   e) Idadi ya Dada: .....
   f) Wewe ni wa ngapi katika familia: .....

Mimi .....(Mwanafunzi) nathibitisha kuwa taarifa nilizojaza hapo juu ni za kweli.

SAHIHI YA MWANAFUNZI:..... TAREHE: .....

Mimi .....(Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi) nathibitisha kuwa taarifa nilizojaza hapo juu ni za kweli.

SAHIHI YA MZAZI/MLEZI: ..... TAREHE: .....

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT AUTHORITY

KAHORORO SECONDARY SCHOOL,
P.O BOX 198,
BUKOBA.

DATE……..

TO MEDICAL OFFICER
……
……..
……..

RE: ……
(**NAME OF STUDENT**)

Please examine the above named as per Medical Examination form below:

……
HEADMASTER.

MEDICAL EXAMINATION FORM:
(To be completed by Medical Officer)

Full Name……..

Age……**Height**:……(**Weight**……**Kg**)

1. Blood count:……
2. Stool examination:……
3. Urinalysis:……
4. Pyphilias and other V.d:……
5. T.B. and leprosy test:……
6. Eye test:……
7. Ear:……
8. Chest:……..
9. Abdomen:……..
10. Plamo test: (Gerls):……..
11. Spleen:……

12. ADDITIONAL INFORMATION

E.g. Physical defects of impairments, infections, chronic or family disease (e.g) sickle cell, inability to eat certain foods ets.

……

……

I have examined the above named student and A certify that he is **FIT/ NOT FIT** to persue Secondary Education.

Signature:…… Station:……

Designation:…….. Date:……..

N.B: **Mzazi unaombwa kumkatia kijana wako Bima ya Afya ili kurahisisha matibabu pindi anapougua na kulazimika kupelekwa hospitalini.**

VITABU NA VIFAA VYA KUJIFUNZIA:

Kwa sababu mwanafunzi anakuja hapa kwa lengo la kusoma, katika bodi ya Shule tulikubaliana kuwa kila mwanafunzi awe na:-

(i) Madaftari makubwa ya kutosha.
(ii) Calculator – kwa wale wanao soma masomo ya sayansi + Hesabu (Scientifi culcuator).
(iii) Karatasi za graph zinazotosha.
(iv) Kalamu, rula, Advanced Dictionary.
(v) Pia mwanafunzi awe na vitabu vya kujisomea. Tumeorodhesha vitabu kwa kila somo ambavyo mzazi / mlezi unatakiwa umnunulie angalau kitabu kimoja kwa kila somo. Hii ni kwa sababu vitabu vya shule havitoshelezi idadi ya wanafunzi tulionao. Lakini ukipata kitabu kingine cha A'level umpatie ilimradi akifika kitakaguliwa na walimu wa masomo kuona kama kinafaa. Hivi vitabu ni mali ya mwanafunzi, ataondoka navyo baada ya kumaliza masomo kwa ajili ya wadogo/ndugu zake wengine. Kwa hili tunakuomba utupe ushirikiano. Endapo hutapata hivi vitabu kutokana na sehemu uliyopo labda hakuna maduka ya vitabu basi siku ya kuripoti mwanafunzi afike na hela ataelekezwa sehemu ya kuvitafuta, au wasiliana na wakurugenzi wa maduka ya vitabu haba Bukoba.

(a) S.S. MUNYAHI INTERPRISE
P.O.BOX
BUKOBA.
SIMU NO: 0765-325476

(b) EDICOM INTERPRISE
P.O. Box..
BUKOBA.
SIMU NO. 0688-858885

(c) CHURCH BOOKSHOP
P.O.BOX …
BUKOBA.
(066) 20954

ORODHA YA VITABU MWANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO ANAVYOTAKIWA KUWANAVYO (ITAKUWA NI MALI YAKE):-

SOMO	JINA LA KITABU	MWANDISHI	TOLEO	MAONI
CHEMISTRY	1.A-level Chemistry	E.N. Ramsden	4th Edition	-Topiki zote
	2.Physical chemistry	Mark Daniel		General & Physical
	3.Inorganic Chemistry	Mzumbe books project	Part I and Part II	Soil & Environmental chem.
PHYSICS	1. Pricnciples of Physics for class XI	V.K.Mehta (S. Chand)	Revised Edition	
	2. Pricnciples of Physics for class XII	V.K.Mehta (S. Chand)	Revised Edition	
	3. University Physics with Modern Physics	Young and Freedom	12th Edition	
	4.Advanced Level Physics	Tom Duncan	4th Ed.	
	5.Advanced Level Physics	Nelkon & Parker	5th & 7th Ed	
	6.Advanced Level Physics	Roger Muncoster		
	1. Biological science	R.Soper	3rd Edition	

BIOLOGY	2. New understanding Biology	P.O. Green & Nelson Thomas	Third edition 4th edition	
ADV.MATHS	1. Understanding pure math	A.J.Sadler		
	2. Mathematics for class X I	S.Chand		
	3. Mathematics for Class XII	S.Chand		
HISTORY	1. Mastering Adv.Level.PP.1	Kato, A.	2 nd ed.	
	2. Oxford Advanced Learners		1st ed.	
	History.	Oxford.	1st ed.	
	3. History Part II Alive	Zisti, K		
GEOGRAPHY	1. Monkhouse (Physical Geography)	Monkhouse		
	2. Geography an integrated	David Waugh		
	3. Approved 4th ed.			
ECONOMICS	1. Economics Simplied	N.A Salemi		
	2. Modern Economics	- R. Madida.		
	3. Micro – Economics	- Ambilikile.		
KISWAHILI	1. Kiswahili 1, Nadharia ya lugha, Kidato cha 5 & 6.	By Masuko Christopher		
	2. Kiswahili 2, Nadharia ya Fasihi. Kidato cha 5 & 6.			
	3. Tasfiri na ukalimani	By Pr. Mansoko		
BAM	1. Pure and Applied Math's	C.J.Tranter		
	2. Advance Math 1	C.W.Celia		
GENERAL STUDIES	1. General studies Notes	-Nyambari C.Nyanguwine. Godfrey R. Bukagile & Stephen O.Maluka - 2009		
	2. General studies supplementary book for A – level and colleges.	Civic education Teachers association (CETA) -2010		
ENGLISH	Advanced English Language Form 5 & 6	James John (Oxford univ.Press	1st Ed.	

<u>NB</u>: Mwanafunzi apate Kitabu kimoja kila somo au zaidi kutokana na uwezo mzazi / mlezi.